Tanganyika Law Society

IJUE SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA YA MWAKA 2017 KATIKA LUGHA RAHISI

UCHAMBUZI WA SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA YA MWAKA 2017



FEBRUARI, 2019

KIMEANDALIWA NA
Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara
Kiwanja Na. 391, Mtaa wa Chato
Regent Estate, S.L.P 2148
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 2775313/ +255 22 5500002
Nukushi +255 22 2775314
Barua Pepe info@tls.or.tz
Tovuti www.tls.or.tz

© Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara, 2019

Mwandishi
Mackphason Buberwa

Wahariri
Stephen Msechu,
Mabhezya Rehani
Kaleb Lameck Gamaya

Kimeandaliwa na kuhaririwa chini ya usimamizi wa
Kamati ya Masuala ya Katiba na Sheria

Mpale Mpoki
Harold Sungusia
John Seka
Stephen Mwakibolwa
Daimu Khalifani
Elizabeth Mhagama
Paul Kaunda

YALIYOMO

SHUKRANI 2
UTANGULIZI 4
SURA YA KWANZA 5
1.1 MALENGO YA KUTUNGWA KWA SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA YA MWAKA 2017 5
SURA YA PILI 6
2.1 SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA KWA KIFUPI 6
SURA YA TATU 8
3.1: MAENEO NA VITU MUHIMU VYA KUZINGATIA KATIKA SHERIA HII 8
3.2: VYOMBO VYA URATIBU WA SHUGHULI ZA UTOAJI WA MSAADA WA KISHERIA VILIVYOUNDWA CHINI YA SHERIA HII 9
SURA YA NNE 13
4.1 USAJILI WA WATOA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA 13
4.2 KUKUBALIWA AU KUKATALIWA KWA MAOMBI YA UTOAJI MSAADA WA KISHERIA 14
4.3 TARATIBU ZA RUFAA ENDAPO MAOMBI YAMEKATALIWA 14
4.4 USIMAMIZI WA NIDHAMU NA UWAJIBIKAJI KWA WATOA MSAADA WA KISHERIA 15
SURA YA TANO 18
5.1 MASUALA NA MASHARTI MAALUM KWA WASAIDIZI WA KISHERIA 18
SURA YA SITA 21
6.1 UTOAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA NA MASHARTI YAKE 21
6.2 SIFA NA WAJIBU WA MTOA HUDUMA ZA KISHERIA 22
6.3 MSAADA WA KISHERIA KWA WATOTO WALIOKINZANA NA SHERIA 24
SURA YA SABA 26
HITIMISHO 26

SHUKRANI

Kamati ya Katiba na Masuala ya Sheria pamoja na Kamati ya Msaada wa Kisheria za Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara zilizobeba dhamana ya kufanya uchambuzi na kutoa mapendekezo juu ya Muswada wa Sheria ya Msaada wa Kisheria wa Mwaka 2017, zinatoa shukrani zao za dhati kwa watu na taasisi zote zilizohusika katika mchakato wa kutunga sheria hii muhimu ya Msaada wa Kisheria. Kipekee tunampongeza mheshimiwa **Angela Jasmin Kiruki**; ndugu **Joseph Ndunguru** na **bi. Felistas Mushi** kwa uongozi bora tangu hatua za awali za mchakato wa kupatikana kwa Muswada huu. Pia tunatambua mchago wa mashirika na asasi za kiraia zilizoshiriki katika Mchakato wa kupata Muswada na Sheria hii.

Kipekee kamati zinatoa shukrani zao kwa Baraza la Uongozi la Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara kwa Imani yao kwa kamati hizi na rasimali walizozitoa kuwezesha kamati hizi kutekeleza majukumu yao.

Kwa namna ya kipekee, kamati zinatoa shukrani zake kwa aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa **Dr. Harrison G. Mwakyembe** kwa mchango wake mkubwa wa kutoa fursa kwa wadau mbalimbali kutoa mawazo yao kwa ajili ya kuboresha muswada wa sheria ya msaada wa kisheria na utayari wake na wizara yake wa kila mara kushirikiana na wadau mbalimbali kujadili muswada kwa mapana kwa nia ya kuuboresha ili kupata sheria nzuri kwa maslahi ya taifa letu.

Shukrani zinatolewa pia kwa Kamati ya Bunge ya Katiba na Masuala ya Sheria kwa kuzipa kamati pamoja na wadau mbalimbali fursa ya kufika mbele ya kamati ya Bunge kuwasilisha na kuelezea mapendekezo yao juu ya muswada wa sheria ya

msaada wa kisheria kwa ajili ya kuuboresha zaidi muswada kwa maslahi ya taifa letu. Kamati zinaipongeza sana kamati ya bunge ya katiba na masuala ya sheria kwa kupokea na kufanyia mapendekezo mengi ya Chama cha Wanasheria Tanzania Bara na wadau wengine kwa ajii ya kuuboresha muswada mpaka kupatikana kwa sheria ya msaada wa kisheria ya mwaka 2017.

Mwisho, kamati zinatoa shukrani kwa wawakilishi wa mashirika ya kiraia na wadau wengine mbalimbali kwa ushirikiano wao katika kuchambua na kuwasilisha mapendekezo yao juu ya muswada wa sheria hii.

UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Katiba na Sheria iliwasilisha Muswada wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza.

Bunge kupitia kamati yake ya kudumu ya Katiba na Masuala ya Sheria iliwaalika wadau mbalimbali ikiwemo Chama cha Wanasheria Tanzania Bara kutoa mapendekezo yao juu ya muswada huo.

Chama cha Wanasheria Tanzania Bara kupitia kamati zake za Katiba na Masuala ya Sheria na Kamati ya Msaada wa Kisheria zikishirikiana na wadau wengine mbalimbali kiliwakilisha maoni yake kwa kamati ya kudumu ya Bunge ya Katiba na Masuala ya Sheria. Kamati ya Bunge iliyapokea maoni hayo na kuyafanyia kazi kisha kupeleka ripoti yake bungeni ambapo ripoti hiyo ilijadiliwa na Bunge kuipitisha sheria hii kwa kuzingatia kwa kiasi kikubwa maoni yaliyotolewa na wadau mbalimbali kikiwemo Chama cha Wanasheria Tanzania Bara.

Sheria hii ya msaada wa kisheria imetiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. John Pombe Joseph Magufuli mnamo tarehe 21 Februari, 2017 ili kukamilisha taratibu za utungwaji wa Sheria hii.

Kutokana na umuhimu wa sheria hii, Chama cha Wanasheria Tanzania Bara kimeona ni vyema kuandika kijitabu hiki kwa lengo la kuiweka sheria hii katika lugha rahisi kabisa kwa mtu yeyote ambaye hana taaluma ya uanasheria anaweza kuielewa sheria hii na pia kuonyesha maeneo muhimu ya sheria hii kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wake hususani kwa kuwalenga wasaidizi wa kisheria.

SURA YA KWANZA

1.1 MALENGO YA KUTUNGWA KWA SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA YA MWAKA 2017

Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria ambayo ndio wizara yenye dhamana ya kusimamia utolewaji huduma za kisheria nchini, ilipeleka Muswada wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017 kwa malengo makuu matatu. Malengo hayo ni pamoja na;

1. Kuanzisha mfumo wa kisheria utakaosimamia na kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za huduma za kisheria kwa malipo kutoka kwa mawakili
2. Kuwatambua wasaidizi wa kisheria na,
3. Kufuta sheria ya Msaada wa Kisheria (katika mashauri ya Jinai)

Aidha, Wizara ilipendekeza muswada wa sheria hii kutokana na kwamba serikali kwa muda mrefu imekuwa ikitoa msaada wa kisheria kwa watuhumiwa wanaoshitakiwa kwa makossa makubwa tu kama vile mauaji, kuua bila kukusudia na uhaini. Kwa sheria hii mpya, huduma ya msaada wa kisheria itakuwa ikitolewa katika makosa yote ya jinai na ambayo sio jinai.

Pia asasi za kiraia zimekuwa zikitoa huduma ya msaada wa kisheria bila kuwepo utaratibu wa kisheria baina ya taasisi hizo na serikali. Sheria hii inalenga kuondoa ombwe hilo kwa kuweka mfumo madhubuti na endelevu ili kutoa suluhisho la changamoto zilizopo na kuhakikisha kuwa huduma ya msaada wa kisheria nchini inaleta matokeo chanya kwa ustawi wa wananchi, hususani wa vijijini na wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za mawakili.

"*msaada wa kisheria*" au "*huduma ya kisheria*" inayojumuisha utoaji wa ushauri wa kisheria, usaidizi wa kisheria au uwakilishi kwa watu wasiokuwa na uwezo



SURA YA PILI

2.1 SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA KWA KIFUPI

Sheria hii imegawanyika katika sehemu kuu saba kama ifuatavyo; **Sehemu ya Kwanza** ya Sheria inajumuisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la Sheria, matumizi na tasfiri ya misamiati na maneno mbalimbali yaliyotumika katika Sheria hii.

Sehemu ya Pili inaweka masharti ya usimamizi na uratibu wa watoa huduma ya msaada wa kisheria. Sehemu hii inaanzisha Bodi ya Ushauri ya Huduma ya Msaada wa Kisheria na kuainisha majukumu yake. Vilevile, inaweka utaratibu wa uteuzi wa Msajili na majukumu yake.

Sehemu ya Tatu inaweka masharti ya usajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria, inaainisha sifa za kusajiliwa kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria, utoaji wa cheti cha usajili mara baada ya kusajiliwa kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria, mazingira yanayoweza kupelekea kusitishwa au kufutwa kwa cheti cha usajili. Sehemu hii pia inaainisha haki ya rufaa dhidi ya uamuzi wa kusitishwa au kufutwa kwa cheti. Vilevile, sehemu hii inaweka masharti ya uteuzi wa Msajili Msaidizi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

Sehemu ya Nne inaainisha masharti mahususi kwa wasaidizi wa kisheria, sifa, majukumu na masharti ya wasaidizi wa kisheria kutoa ushauri na usaidizi wa kisheria kwa mujibu wa masharti ya sheria hii. Pia inaweka katazo kwa wasaidizi wa kisheria kutoza ada kwa mtu anayesaidiwa na kutojihusisha na shughuli zilizotengwa kwa ajili ya mawakili.

Sehemu ya Tano inaainisha masharti ya mtu anayeweza kuomba huduma ya msaada wa kisheria, masharti ya jumla ya huduma ya msaada wa kisheria, huduma ya msaada wa kisheria katika mashauri ya madai na jinai kwa amri ya mahakama. Pia sehemu

hii inatoa masharti ya upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watoto na watu walio katika vituo vya polisi, magereza na vizuizi mbalimbali.

Sehemu ya Sita inahusu masharti ya fedha. Masharti hayo yanajumuisha vyanzo vya mapato ya Bodi ilianzishwa kusimamia utolewaji wa huduma ya msaada wa kisheria, makadirio ya mwaka na vitabu vya hesabu. Vilevile, inaainisha mamlaka ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua hesabu za Bodi.

Sehemu ya Saba inaainisha masharti mengineyo ya ujumla. Masharti hayo yanajumuisha mamlaka ya Msajili kutoa tangazo kwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria kudhibitisha uwepo wake (uhai wa ofisi yake), wajibu kuhusiana na miiko ya maadili ya kitaaluma kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria na mamlaka ya Waziri mwenye dhamana kutunga kanuni za maadili ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria. Vilevile, sehemu hii inaainisha masharti ya kuifuta Sheria ya Msaada wa Kisheria katika Mashauri ya Jinai, Sura ya 21 na kuanisha Masharti yatokanayo na masharti ya mpito.

SURA YA TATU

3.1: MAENEO NA VITU MUHIMU VYA KUZINGATIA KATIKA SHERIA HII

a) Kuanza kutumika kwa Sheria

Kwa mujibu wa sheria hii, kifungu cha kwanza kinasema kwamba sheria hii itaanza kutumika tarehe ambayo waziri mwenye dhamana atateua kupitia Tangazo la Serikali litakalochapishwa kwenye gazeti la Serikali. Kwa mujibu wa kifungu cha pili cha sheria hii, sheria hii itatumika Tanzania Bara tu.

b) Baadhi ya Misamiati na Maneno Yaliyotumika katika Sheria hii na Tafsiri zake Kisheria

"*wakili*" maana yake ni wakili anayefanya kazi za uwakili kwa mujibu wa sheria ya Mawakili;

"*mtu anayesaidiwa*" maana yake ni mtu anayepatiwa msaada wa kisheria chini ya Sheria hii;

"*Msajili Msaidizi*" maana yake ni Msajili Msaidizi atakayeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha sheria hii;

"*Bodi*" maana yake ni Bodi ya Taifa ya Ushauri ya Huduma ya Msaada wa Kisheria iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha sheria hii;

"*Mtendaji Mkuu wa Mahakama*" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Mahakama aliyeteuliwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mahakama;

"*mtu asiye na uwezo*" maana yake ni mtu asiye na uwezo wa kumudu gharama za wakili wa kujitegemea na inajumuisha makundi mengine ya watu kama itakavyohitajika kwa maslahi ya utoaji haki;

"*ushauri na msaada wa kisheria*" maana yake ni ushauri na msaada unaotolewa kwa mtu asiye na uwezo katika kesi za jinai na madai juu ya sheria fulani, taratibu za kisheria na uandaaji wa nyaraka za kisheria;

"*msaada wa kisheria*" au "*huduma ya kisheria*" inajumuisha utoaji wa ushauri wa kisheria, usaidizi wa kisheria au uwakilishi kwa watu wasiokuwa na uwezo;

"*mtoa huduma ya msaada wa kisheria*" maana yake ni mtu au taasisi iliyosajiliwa chini ya Sheria hii kutoa huduma ya msaada wa kisheria;

"*Waziri*" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya Sheria (Waziri wa Katiba na Sheria);

"*msaidizi wa kisheria*" maana yake ni mtu anayetoa huduma ya msaada wa kisheria kwa mujibu wa sheria hii;

"*Katibu Mkuu*" maana yake ni Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na mambo ya Sheria (Wizara ya Katiba na Sheria);

"*Msajili*" maana yake ni msajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria atakayeteuliwa chini ya kifungu cha 6 cha sheria hii na;

"*Rejesta*" maana yake ni Rejesta(orodha) ya watoa huduma ya msaada wa kisheria iliyoanzishwa chini ya sheria hii.

3.2: VYOMBO VYA URATIBU WA SHUGHULI ZA UTOAJI WA MSAADA WA KISHERIA VILIVYOUNDWA CHINI YA SHERIA HII

3.1.1 Bodi ya Taifa ya Ushauri ya Msaada wa Kisheria

Kifungu cha 4 cha sheria hii kinaanzisha Bodi ya Taifa ya Ushauri ya Msaada wa Kisheria.

a) Kazi za Bodi

Kazi za Bodi hii zimeainishwa katika kifungu cha 5 ambazo ni pamoja na;

i. Kutoa miongozo ya kisera kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria;
ii. Kumshauri Waziri juu ya masuala ya kisera na mambo mengine yahusianayo na uboreshaji wa utoaji wa huduma ya msada wa kisheria;
iii. Kuthibitisha taarifa yam waka ya watoa huduma ya msaada wa kisheria;
iv. Kuamua rufaa zinazotokana na uamuzi wa Msajili na;

v. Kutekeleza majukumu mengine kadri itakavyoelekezwa na Waziri

Katika kutekeleza majukumu yake, Sheria inaitaka Bodi kudumisha kwa kadri inavyowezekana mfumo wa mashauriano na ushirikiano kati yake na Wizara, taasisi za serikali, watoa huduma ya msaada wa kisheria au vyombo vingine vya umma au binafsi vilivyoanzishwa na sheria yoyote ya Bunge.

b) Wajumbe wa Bodi

Wajumbe wa Bodi hii wameainishwa katika Jedwali la sheria hii, ikiwa ni pamoja na;

i. Mwenyekiti ambaye atakuwa Jaji wa Mahakama Kuu atakayeteuliwa na Waziri kwa kushauriana na Jaji Mkuu;
ii. Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mwakilishi wake mwenye cheo cha ngazi si chini ya Afisa wa Sheria;
iii. Mwakilishi kutoka taasisi za watoa huduma ya msaada wa kisheria;
iv. Mwakilishi kutoka Jukwaa la Taifa la Haki Jinai
v. Mwakilishi kutoka Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara
vi. Mkurugenzi wa Sheria kutoka wizara yenye dhamana na Serikali za Mitaa
vii. Mwakilishi wa watu wenye ulemavu; na
viii. Mwakilishi kutoka taasisi zinazowakilisha wasaidizi wa kisheria

c) Uwiano wa Kijinsia

Kwa kutambua uwiano wa jinsia katika Bodi hii, sheria imeweka sharti kwamba mamlaka ya uteuzi katika kuteua wajumbe wa Bodi hii itahakikisha kuwa kuna uwakilishi wa kijinsia katika Bodi. Makamu mwenyekiti wa Bodi hii atachaguliwa na wajumbe kutoka miongoni mwao.

d) Muda wa Bodi

Muda wa kuwa madarakani kwa wajumbe wa Bodi hii utakuwa ni miaka mitatu na watakuwa na sifa ya kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

e) Akidi na Taratibu za Mikutano ya Bodi

Akidi katika mkutano wowote wa Bodi inatakiwa kuwa na angalau wajumbe watatu. Maamuzi ya vikao vya Bodi yataamuliwa kwa uwingi wa kura za wajumbe waliohudhuria na kupiga kura. Ikitokea kuna usawa wa kura, mtu anayeongoza mkutano atakuwa na kura ya uamuzi wa pili ili kuondoa usawa katika kura za awali. Sheria inatoa fursa pia kwa maamuzi ya Bodi kufanyika bila mkutano kwa njia ya kusambaza karatasi au nyaraka husika miongoni mwa wajumbe ijapokuwa mjumbe yeyote ana haki ya kuomba suala hilo likajadiliwe kwenye Mkutano wa Bodi.

3.2.2 Msajili wa Watoa wa Msaada wa Kisheria

Kifungu cha 6 cha Sheria hii kinatamka kwamba kutakuwa na Msajili wa watoa huduma ya Msaada wa Kisheria. Msajili huyu atakuwa ni Mkurugenzi anayehusika na masuala ya Msaada wa Kisheria katika Wizara ya Katiba na Sheria.

a) Kazi za Msajili

Kazi za msajili wa watoaji msaada wa kisheria zimeainishwa katika kifungu namba 7 ikiwa ni pamoja na;

i. Kusajili watoa huduma ya msaada wa kisheria;
ii. Kuchunguza malalamiko ya ukiukwaji wa maadili, uzembe, utovu wa nidhamu au kutotii dhidi ya watoa huduma za msaada wa kisheria;
iii. Kusitisha au kufuta usajili wa mtoa huduma yeyote wa msaada wa kisheria;
iv. Kuhifadhi na kutunza daftari la orodha ya watoa huduma ya msaada wa kisheria;
v. Kukagua ofisi yoyote ya mtoa huduma ya msaada wa kisheria kwa lengo la kujiridhisha na ubora wa huduma ya msaada wa kisheria inayotolewa;
vi. Kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kukuza uelewa na ufahamu wa masuala ya kisheria kwa umma hususani kuelimisha makundi ya wanyonge kuhusu haki na wajibu chini ya Katiba na sheria nyingine;
vii. Kuratibu na kuwezesha uazishwaji na utambuzi wa mitaala kwa ajili ya mafunzo ya wasaidizi wa kisheria kwa kushauriana na watoa huduma ya msaada wa

kisheria pamoja na mamlaka za utoaji leseni za elimu;

viii. Kuratibu, kufuatilia na kutathmini kazi za watoa huduma ya msaada wa kisheria na kutoa miongozo ya jumla na mahsusi kwa utelekezaji bora wa programu za huduma ya msaada wa kisheria;

ix. Kutunza kumbukumbu na taarifa kuhusu watoa huduma ya msaada wa kisheria;

x. Kuandaa taarifa mbalimbali kuhusu huduma ya msaada wa kisheria na masuala mengine ya kuwasilisha kwenye Bodi;

xi. Kuwezesha ushirikishwaji wa taarifa kwa njia rafiki na kutoa miongozo ya kimahusiano baina ya watoa huduma za msaada wa kisheria na Serikali;

xii. Kutolea uamuzi migogoro baina ya watoa huduma ya msaada wa kisheria isipokuwa mawakili, na migogoro baina ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wapewa huduma ya msaada wa kisheria; na

xiii. Kufanya kazi nyingine yoyote kama atakavyoelekezwa na Waziri au Bodi.

b) Wasaidizi wa Msajili

Katika utendaji wake wa kazi Msajili atasaidiwa na maafisa wengine ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria na atakuwa akiwajibika kwa Katibu Mkuu wa Wizara ambaye ametajwa kama kiungo kati ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na Serikali.

Kwa kuwezesha usajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria katika ngazi ya mikoa na wilaya, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushauriana na mamlaka mbalimbali husika atateua katika kila mkoa au wilaya mtumishi wa umma kutoka miongoni mwa watumishi wa umma ndani ya mkoa au wilaya kuwa Msajili Msaidizi. Hii inamaanisha kwamba watoa huduma ya msaada wa kisheria walioko mikoa mingine tofauti na Dar es salaam au Dodoma hawatalazimika kusafiri kwenda Dar es Salaam au Dodoma kwa ajili ya usajili wao.

SURA YA NNE

4.1 USAJILI WA WATOA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA

Sheria hii inaweka masharti kwamba taasisi yoyote inayotaka kutoa msaada wa kisheria isajiliwe kwa mujibu wa sheria hii.

4.1.1 Sifa za Watoa Msaada wa Kisheria

Taasisi hiyo itasajiliwa endapo itakuwa na sifa zifuatazo;

a) Imesajiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi;
b) Utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria ni moja ya majukumu yake ya msingi;
c) Ina majengo ya ofisi na vifaa vya ofisi;
d) Ina si chini ya:
    i. Mawakili wawili;
    ii. Wakili mmoja na mwanasheria mmoja;
    iii. Mwanasheria mmoja na wasaidizi wa kisheria wawili; au
    iv. Wasaidizi wa kisheria watatu; na
e) Imepitishwa na taasisi iliyoisajili kuhusu kumbukumbu zake za usimamizi wa fedha.

4.1.2 Rejesta ya Watoa Msaada wa Kisheria

Sheria hii pia inamtaka Msajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria kuwa na rejesta ya majina yote ya taasisi zilizosajiliwa kama watoa huduma ya msaada wa kisheria. Rejesta au orodha hiyo itachapwa katika nakala mango au nakala tete na itatakiwa kupatikana kwa umma katika vituo vya polisi, mahakama, magereza na maeneo mengine kama itavyoamuliwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

4.1.3 Utaratibu wa Kuomba kuwa Mtoa Msaada wa Kisheria

Maombi ya usajili yatafanyika kupitia fomu maalumu kama ilivyoanishwa katika Jedwali la kwanza la Kanuni za Sheria hii. Maombi hayo yanatakiwa kuambatanishwa na;

a) Nakala ya katiba ya taasisi hiyo au nyaraka yoyote

iliyoianzisha;

b) Taarifa binafsi za wenye ofisi, mawakili au wasaidizi wa sheria;

c) Taarifa zinazohusu anwani ya eneo yalipo makao makuu ya taasisi hiyo;

d) Nakala ya hati safi kutoka mamlaka ya usajili wa mtoa huduma ya msaada w kisheria;

e) Ada ya usajili itakayokuwa imebainishwa kwenye kanuni za sheria hii; na

f) Maelezo au taarifa nyingine kama zitavyohitajika na Msajili.

4.2 KUKUBALIWA AU KUKATALIWA KWA MAOMBI YA UTOAJI MSAADA WA KISHERIA

a) Taarifa baada ya maombi kupelekwa kwa msajili

Kama maombi yatakamilika kwa mujibu wa sheria na kanuni za sheria hii, Msajili atatakiwa ndani ya siku 21 kutoa majibu ya aidha maombi yamekubaliwa au yamekataliwa. Endapo maombi hayo yatakuwa yamekataliwa, sheria inamtaka Msajili kutoa sababu zakukataliwa kwake na kumtaarifu mwombaji juu ya kukataliwa kwa maombi yake.

b) Sababu za Kukataliwa kwa Maombi

Ni muhimu kutambua kwamba maombi yanaweza kukataliwa endapo hayatatimiza masharti kwa mujibu wa sheria hii na kanuni zake, au kama taasisi husika imetoa taarifa za uongo au za kupotosha kwa namna yoyote ile wakati wa kufanya maombi yake.

4.3 TARATIBU ZA RUFAA ENDAPO MAOMBI YAMEKATALIWA

a) Muda na Utaratibu wa Kuwasilisha Rufaa

Kama taasisi iliyoomba kusajiliwa haitaridhika na maamuzi ya msajili ya kutoisajili, taasisi hiyo inaweza kukata rufaa kwa Msajili (kama maamuzi yanayokatiwa rufaa yalitolewa na Msaidizi wa Msajili), kwa Bodi (kama maamuzi yanayokatiwa rufaa yalitolewa na Msajili) na kwa Waziri wa Katiba na Sheria (kama maamuzi yanayokatiwa rufaa yalitolewa na Bodi).

b) Muda na Matokeo ya Rufaa
Sheria imeweka muda wa siku 30 wa kukata rufaa katika ngazi zote tajwa hapo juu toka siku ambayo uamuzi unaokatiwa rufaa ulitoka. Sheria pia inampa masharti Waziri kutolea uamuzi rufaa zinazomfikia ndani ya siku 30 kutoka siku aliyopokea rufaa hizo. Rufaa zinazoshindwa kutolewa uamuzi katika ngazi ya Waziri au ikitokea mrufani hakuridhika na maamuzi ya Waziri, basi rufaa hiyo itakwenda Mahakam Kuu ya Tanzania kwa uamuzi zaidi.

4.4 USIMAMIZI WA NIDHAMU NA UWAJIBIKAJI KWA WATOA MSAADA WA KISHERIA

a) Utambulisho na Uthibitisho wa Uhalali wa Mtoa Msaada wa Sheria
Baada ya usajili kukamilika, taasisi inayotoa msaada wa kisheria itapewa cheti cha usajili na Msajii au Msajili Msaidizi.

b) Hatua za awali za Kuwawajibisha Watoa Msaada wa Kisheria
Sheria inatamka kwamba Msajili anaweza kutoa onyo la maandishi, kusitisha au kufuta kabisa cheti cha usajili cha mtoa huduma ya msaada wa kisheria.

c) Sababu za Kusitisha Usajili wa Watoa Msaada wa Kisheria
Msajili anaweza kusitisha cheti cha usajili cha mtoa huduma ya msaada wa kisheria pale ambapo atajiridhisha kwamba;

i. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria ametenda kosa la kitaaluma au ameshindwa kumchukulia hatua za kinidhamu mtumishi wake kwa kukiuka taratibu za kitaaluma au kukiuka maadili yaliyowekwa na chombo husika cha kitaaluma;
ii. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria amekiuka miiko ya kinidhamu iliyoainishwa chini ya Sheria hii au chini ya sheria nyingine yoyote;
iii. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria anatekeleza majukumu yake kinyume na katiba yake; au
iv. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria ameshindwa kuhifadhi kumbukumbu sahihi za kazi zilizofanywa kwa niaba ya mtu aliyesaidiwa na Msajili anaona

kwamba kitendo hicho kitaathiri maslahi ya mtu aliyesaidiwa kwa ujumla au kwa namna nyingine yoyote.

d) Sababu za Kufutwa kwa Usajili wa Mtoa Msaada wa Kisheria.

Msajili pia anaweza kufuta kabisa cheti cha usajili cha mtoa huduma ya msaada wa kisheria iwapo ataridhika kwamba;

i. Usajili umepatikana kimakosa, kwa udanganyifu, kwa ujanja, ushawishi usio halali au kwa taarifa za kupotosha;
ii. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria ameshindwa kutimiza masharti ya usajili;
iii. Sifa za kusajiliwa zimekoma kwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria;
iv. Mwenye ofisi ya mtoa huduma ya msaada wa kisheria ametangazwa kufilisika, amefilisiwa au ameingia katika makubaliano na wadeni wake;
v. Wakili au msaidizi wa kisheria aliyeajiriwa na mtoa msaada wa kisheria amekuwa akikiuka mara kwa mara maadili ya kitaaluma;
vi. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria amekuwa akitoa huduma kwa misingi ya ubaguzi wa jinsia, dini, rangi, kabila au siasa;
vii. Mwenye ofisi ya kutoa huduma za msaada wa kisheria ametiwa hatiani kwa makosa yanayohusu uadilifu, uwajibikaji wake au amepewa amri chini ya chombo husika; au
viii. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria hatoi, au hajatoa huduma ambayo amesajiliwa kuitoa kwa kiwango kilichowekwa.

e) Masharti ya Jumla Kuhusiana na Nidhamu na Uwajibikaji wa Watoa Msaada wa Kisheria

Sheria inamtaka Msajili kutositisha au kufuta cheti cha usajili cha mtoa huduma pale ambapo mtoa huduma ameweza kuchukua

hatua stahiki kurekebisha yale yote ambayo yangepelekea kusitishwa au kufutwa kwa cheti chake.

Msajili akisitisha au kufuta cheti cha usajili, atamtaarifu mtoa huduma ya msaada wa kisheria kuhusu uamuzi wake na kuamuru mtoa huduma za msaada wa kisheria husika kuacha kufanya kazi hiyo au anaweza kuondoa jina lake kwenye Rejesta kama ataona inafaa kufanya hivyo.

SURA YA TANO

5.1 MASUALA NA MASHARTI MAALUM KWA WASAIDIZI WA KISHERIA

Sheria inatoa tafsiri ya msaidizi wa kisheria kama mtu ambaye ameidhinishwa na kudhibitishwa kutoa msaada wa kisheria baada ya kupata mafunzo maalum ya msaidizi wa kisheria yaliyoidhinishwa na mamlaka husika kutoka taasisi inayotambulika kisheria.

5.2 Sifa za Watoa Msaada wa Kisheria

Sheria imeweka sifa na vigezo vya mtu kuwa msaidizi wa kisheria. Sheria inasema msaidizi wa kisheria atatakiwa kuwa na moja kati ya sifa navigezo vifuatavyo;

a) Shahada ya fani yoyote kutoka katika chuo kinachotambulika kisheria;
b) Stashahada au Astashahada ya fani yoyote kutoka katika chuo kinachotambulika kisheria; au
c) Cheti cha elimu ya sekondari.

Ni muhimu kutambua kwamba pamoja na sifa zilizoainishwa hapo juu, msaidizi wa kisheria atatakiwa kuwa amepata mafunzo maalum ya wasaidizi wa kisheria.

5.3 Hatma ya Wasaidizi wa Kisheria Waliokuwepo Kabla ya Kutungwa kwa Sheria Hii

Sheria imewatambua wasaidizi wote wa kisheria waliopo sasa kabla kutungwa kwa sheria hii. Masharti yaliyowekwa na sheria hii ni kwamba msaidizi wa kisheria anayetambulika ni yule ambaye amekuwa akifanya kazi ya msaidizi wa kisheria katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kabla ya kutungwa sheria hii na awe alipata mafunzo maalum ya wasaidizi wa kisheria kutoka kwa taasisi inayotambulika kisheria.

5.4 Majukumu ya Wasaidizi wa Kisheria

Kwa mujibu wa Sheria hii, msaidizi wa kisheria atakuwa na majukumu yafuatayo;

a) Kuendesha mafunzo kwa lugha ya taifa au ya asili kuhusu masuala ya kisheria na taratibu zinazohusu jamii husika;
b) Kumsaidia mtu anayehusika kuhusu taratibu za kupata nyaraka muhimu za kisheria;
c) Kumwelekeza mtu anayesaidiwa njia sahihi ya kupata haki yake; na
d) Kushauri pande zinazopingana kutafuta suluhu ya migogoro au kuwaelekeza kwenye vyombo vinavyohusika na usuluhishi wa migogoro.

5.5 Usajili wa Wasaidizi wa Kisheria

a) Muda na Taratibu za Kusajili Wasaidizi wa Kisheria

Msaidizi wa kisheria atatakiwa kusajiliwa kwa Msajili au Msajili Msaidizi kabla ya kuanza kutoa msaada huduma ya msaada wa kisheria. Hata kwa msaidizi wa kisheria aliyeanza kutoa huduma ya msaada wa kisheria na aliyetambulika chini ya sheria hii, atatakiwa kusajiliwa na Msajili au Msajili Msaidizi kwa mujibu wa sheria hii kabla ya kuendelea kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa jamii.

Baada ya miaka miwili kupita kutoka kuanza kutumika kwa sheria hii, msaidizi wa kisheria ambae atakuwa bado hajasajiliwa na Msajili au Msajili Msaidizi; hatapaswa kutoa huduma ya msaada wa kisheria na atapoteza sifa za kuwa msaidizi wa kisheria.

b) Makosa na Adhabu kwa Watoa Msaada wa Kisheria bila Kusajiliwa

Ni kosa kisheria kwa msaidizi wa kisheria kutoa huduma ya msaada wa kisheria kama hajasajiliwa na Msajili au Msajili Msaidizi kwa mujibu wa sheria hii. Mtu akiuka masharti haya na kukutwa na hatia, atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja za kitanzania au kifungo cha jela kisichopungua miezi mitatu au kupewa adhabu ya vyote viwili (yaani kutozwa faini na kufungwa jela)

c) Katazo la Wasaidizi wa Kisheria Kufanya Kazi za Wakili

Pia sheria hii inaweka masharti ya msaidizi wa kisheria kutojihusisha na shughuli zilizotengwa kwa ajili ya mawakili ikiwa ni pamoja na kutotoza fedha kwa huduma ya msaada wa kisheria atakayokuwa anaitoa.

SURA YA SITA

6.1 UTOAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA NA MASHARTI YAKE

6.1.1 Masharti ya Utoaji huduma za msaada wa kisheria

Sheria imeweka masharti mbalimbali ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa ujumla, katika mashauri ya madai na katika mashauri ya jinai. Sheria hii imetambua msaada wa kisheria katika mashauri ya madai ambayo haikuwa ikitambuliwa na sheria zilizopita. Kwa maana hiyo, sheria hii imepanua wigo wa msaada wa kisheria. Maombi haya yanaweza kufanywa na yeyote kati ya hawa;

(a) mwombaji mwenyewe;
(b) mtu mwingine yeyote aliyeruhusiwa na mwombaji; au
(c) mtu au taasisi yoyote kwa niaba ya mwombaji endapo idhini ya mwombaji ni vigumu kupatikana.

6.1.2 Utaratibu wa Kuomba na Kupata Msaada wa Kisheria

a) Uwasilishaji wa Maombi ya Msaada wa Kisheria

Sheria inamtaka mtu anayehitaji huduma ya msaada wa kisheria kuwasilisha maombi yake kwa taasisi inayotoa msaada wa kisheria, ikiwa ni pamoja na wasaidizi wa kisheria. Maombi ya huduma ya msaada wa kisheria yatafanyika kwa kujaza fomu maalum inayopatikana katika jedwali la kanuni za sheria hii. Fomu hizi pia zinapatikana kwa msajili, msajili msaidizi, taasisi zote za utoaji wa huduma za kisheria, vituo vya polisi na magerezani.

b) Sifa na vigezo vya Mpokea Huduma za Msaada wa Kisheria

Vigezo vitakavyotumika kutathmini kama mtu huyo anastahili huduma ya msaada wa kisheria vitakuwa ni vigezo maalum vilivyowekwa na taasisi husika.

Angalizo:

Sharti limewekwa na sheria katika kifungu cha 44 kwamba, mtoa huduma ya msaada wa kisheria hatatakiwa au hapaswi kumbagua au kumnyima mtu huduma ya msaada wa kisheria kwa sababu zitokanazo na jinsia, dini, rangi, kabila au chama chake cha siasa. Mtoa huduma yeyote atakayekiuka sharti hili na kupatikana na hatia,atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyopungua milioni tano na isiyozidi milioni kumi; au kifungo cha miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja; au adhabu zote mbili (yaani kulipa faini na kifungo jela) kwa pamoja.

6.2 SIFA NA WAJIBU WA MTOA HUDUMA ZA KISHERIA

6.2.1 Sifa za Mtoa Huduma

Sheria hii inaweka sharti kwamba, huduma ya msaada wa kisheria itatolewa tu na mtu ambaye ni wakili, mwanasheria au msaadizi wa kisheria na si mtu mwingine yeyote. Mtu yeyote atakayekiuka sharti hili na kukutwa na hatia atakuwa ametenda kosa na adhabu yake ni faini ya milioni tano au kifungo cha mwaka mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja (yaani faini na kifungo)

6.2.2 Wajibu wa Mtoa Huduma

a) Wajibu wa Kutotoza Fedha

Sheria pia imeweka sharti la kutotoza fedha kwa ajili ya kulipia huduma ya msaada wa kisheria. Kifungu cha 25 cha sheria kinatamka kwamba mto huduma hapaswi kudai, kuomba au kupokea malipo kwa ajili ya huduma anayotoa isipokuwa malipo ambayo yameruhusiwa na sheria hii. Mtu atakayekiuka sharti hili atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia adhabu yake ni faini isiyopungua milioni mbili au kifungo kisichopungua miezi sita; au adhabu zote mbili (yaani faini na kifungo). Pamoja na adhabu hizo, mtu huyo atatakiwa kurudisha fedha zote alizopokea kutoka kwa mwombaji wa huduma ya msaada wa kisheria.

b) Wajibu wa Kuzingatia Maslahi ya Mpewa Huduma

Mtoa huduma anatakiwa kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa weledi na itakayohakikisha inalinda maslahi ya mwombaji wa huduma hiyopia anatakiwa kuweka rekodi au taarifa za watu wote aliyowahudumia na kutuma taarifa hizo kwa msajili kila mwaka au kama itakavyoelekezwa na msajili. Msajili au msadizi wa msajili atafuatilia shughuli zote zinahusiana na utoaji wa msaada wa kisheria kwa watoa huduma hiyo wote, ikiwa ni pamoja kuangalia ubora wa huduma hizo.

6.3 Msaada wa Kisheria katika Mashauri ya Madai na Jinai

Kama ilivyosemwa awali, sheria hii imetoa fursa ya kupata msaada wa kisheria katika mashauri yote ya madai na jinai. Sheria inawataka majaji, mahakimu, wenyeviti wa mabaraza ya usuluhishi kuamuru mtu kupatiwa msaada wa kisheria pale ambapo wanaona mtu huyo hawezi kumudu gharama za huduma za kisheria za mawakili. Pamoja na hayo, sheria imetoa fursa pia kwa watu ambao wako kizuizini kama polisi au magerezakupatiwa msaada wa kisheria. Sheria inawataka wakuu wa vituo vya polisi au magereza kuhakikisha watu wote wanaostahili kupata msaada wa kisheria wanatengenezewa mazingira wezeshi kwa ajili ya watu hao kupata msaada wa kisheria. Hii ni pamoja na kuhakikisha wanapewa fomu maalum za kuomba msaada wa kisheria na kupeleka orodha ya watu wanohitaji huduma hiyo kwa msajili au msaidizi wa msajili ambaye atapeleka orodha hiyo kwa taasisi zinazotoa msaada wa kisheria ili watu hao wapatiwe msaada huo. Kuhakikisha utekelezaji wa sharti hili, sheria inawataka wakuu hao kuandaa ripoti na kuipeleka kwa msajili au msaidizi wa msajili juu ya utekelezaji wa sharti hili.

Sheria inaweka sharti la kutoweka dhamana kwa mtu anayepewa msaada wa kisheria. Kifungu cha 32 kinatamka kwamba mtu anayesaidiwa au anayepatiwa msaada wa kisheria hapaswi au hatakiwi kuweka dhamana ya gharama ya shauri lake wakati wa uendeshaji wa shauri au wakati wa rufaa ya shauri hilo.

6.3 MSAADA WA KISHERIA KWA WATOTO WALIOKINZANA NA SHERIA

Sheria pia imetoa fursa kwa watoto waliokinzana na sheria nyingine yeyote kupatiwa msaada wa kisheria mara moja pale ambapo watatiwa nguvuni na vyombo vya dola.
Sheria imeweka masharti kwamba, watoa huduma wote wanaopokea ufadhili wa kifedha kwa ajili ya kutoa msaada wa kisheria wanatakiwa kutumia fedha hizo kwa ajili ya kutoa msaada wa kisheria tu na si vinginenvyo. Kwa mtoa huduma atakayekiuka sharti hili na kutiwa hatiani, adhabu yake itakuwa ni faini isiyopungua milioni kumi na isiyozidi milioni kumi tano au kifungo jela kwa muda usiopungua miezi sita na usiozidi mwaka mmoja; au adhabu zote mbili kwa pamoja (yaani faini na kifungo jela). Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 45 cha sheria.

6.4 Makosa mbalimbali na adhabu yake

Sheria imeanisha makosa ya jumla katika kifungu cha 46 kwamba mtu yeyote ambaye;

(a) kwa udanganyifu, atasababisha au kuruhusu kuingizwa kwa taarifa yoyote ya uongo au isiyo sahihi katika Rejesta au nakala yake yoyote;
(b) atatoa msaada wa kisheria bila ya kuwa na sifa zilizoainishwa chini ya Sheria hii;
(c) anayetoa taarifa ya uongo au kupotosha kwa nia ya kupata nafuu, faida au manufaa chini ya Sheria hii;
(d) anayejifanya amesajiliwa au anajionesha kuwa amesajiliwa chini ya Sheria hii;
(e) anakataa au anashindwa pasipo sababu za msingi kutokea baada ya kupokea wito wa kuitwa katika shauri na Msajili chini ya sheria hii; na
(f) anamzuia au kumkwamisha mjumbe wa Bodi au Msajili au mtu mwingine yeyote katika kutekeleza mamlaka au majukumu yake chini ya Sheria hii; anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita au vyote kwa pamoja.

6.5 Uhusiano wa Sheria hii na Sheria Nyingine

Kutungwa kwa sheria hii kumesababisha kufutwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria katika Mashauri ya Jinai iliyokuwa ikitumika awali. Aidha, sheria hii mpya imetambua taratibu zote za utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kabla ya kutungwa kwa sheria hii. Kifungu cha 50 kinatamka kwamba; taratibu zote za huduma ya msaada wa kisheria zilizopo hadi tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii zitaendelea na kukamilishwa kama vile Sheria hii haijapitishwa. Hii inamaanisha mashauri yote yataendelea kama kawaida. Sheria hii ilianza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2017.

6.6 Hatma ya Taasisi zilizokuwa zikitoa msaada wa kisheria kabla ya kutungwa kwa Sheria hii

Hata hivyo, kifungu hicho cha 50 kimeweka sharti kwamba; taasisi zote zinazotoa huduma za msaada wa kisheria zitaendelea kutoa huduma mpaka itakapoisha miezi kumi na mbili kutoka tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo zitasitisha kutoa huduma na kuhitajika kujisajili kwa mujibu wa Shera hii. Maana yake ni kwamba taasisi zinazotoa huduma zitaendelea kwa taratibu zilizopo lakini ifikapo Julai 2018 zinatakiwa kujisajili kwa mujibu wa sheria hii mpya na kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa mujibu wa sheria hii mpya. Hii inaenda sambamba na kwa wasaidizi wa kisheria.

Sheria inaongeza pia kwamba, kwa wale watoa huduma ambao tayari walisajiliwa na Jaji Mkuu na kupewa cheti maalum cha kutoa huduma ya msaada wa kisheria, watahesabika kuwa wameshasajiliwa chini ya sheria hii mpya.

SURA YA SABA

HITIMISHO

Kijarida hiki kimebeba maudhui yaliyomo kwenye sheria ya Msaada wa Sheria, 2017. Kimechambua kwa lugha rahisi maudhui ya masharti yatokanayo na sheria hii ili kuweza kumsaidia mtu anayehitaji msaada wa kisheria na mtoa huduma ya msaada wa kisheria popote pale Tanzania.

Kijarida hiki kitatumika na wadau wote katika tasnia ya sheria na msaada wa kisheria katika upatikanaji wa haki Tanzania. Pia kijarida hiki kinatoa mwongozo wa sifa za mtoa huduma za msaada wa kisheria na kinaeleza ni wapi huduma hii inaweza kupatikana. Haki na wajibu wa mtoa huduma na mtu anayehitaji msaada wa kisheria zimeelezwa vyema kwa kutazama mipaka ya kila upande katika upatikanaji wa haki nchini.

Kijarida hiki ni nyenzo muhimu kwa wasaidizi wa kisheria ambao kwa mara ya kwanza wanatambulika katika sheria hapa nchini, hivyo Chama cha Sheria Tanganyika (TLS) inaamini maudhui yaliyoandikwa kwa lugha nyepesi katika kijarida hiki yataongeza tija ya kazi zinazofanywa na wasaidizi wa kisheria na watoa huduma za msaada wa kisheria hapa Tanzania. Pia kitawawezesha watu wasio na uwezo kupata haki kwa misingi sawa na watu wengine wenye kipato fedha.

Tanganyika Law Society

Kijarida hiki kimeandaliwa na kuchapishwa na;
Tanganyika Law Society
P.O Box 2148 Plot No. 391,
Chato Street, Regent Estate.
Dar es Salaam – Tanzania
Email: info@tls.or.tz | Website: www.tls.or.tz

FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
Facilitating Partnerships for Development

Kwa msaada wa;
The Foundation for Civil Society
7 Madai Crescent Ada Estate,
P.O. Box 7192,
Dar es Salaam